AINA ZA MANENO

1. **Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kila kivumishi cha pekee ulichopewa.** (alama 2) i) -Ote ii) –o-ote

2. **Onyesha vihisishi katika sentensi zifuatazo.** (alama 2) i) Sawa sawa tutakutana kesho. ii) Nabii Musa! Eti kifaru hula nyama

3. **Taja aina ya vitenzi vilivyopigiwa mstari chini katika sentensi zifuatazo.** (alama 2) i) Huyu ndiye aliyetukomboa. ii) Baba amekuwa mgonjwa

4. Tunga sentensi yenye mpangilio huu wa kisarufi: I +W + T + N + V. (alama 2½)

5. **Onyesha** aina ya vitenzi katika sentensi.
Wewe umewahi kufika shule ukiwa umechelewa? (alama 2)

6. Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo: (alama 2)
(i) Chakula chote kitaharibika. (ii) Chakula chochote kitaharibika.

7. **Tumia** –amba katika sentensi hii: Ua limealo huwa limetiwa mbolea.
(alama 1)

8. **Tambua** aina za maneno katika sentensi ifuatayo:
Walicheka sana walipoambiwa hadithi hiyo. (alama 2)

9. **Tunga** sentensi ukitumia semi zifuatazo:(i) Kula uhondo (al 2) (ii) Regea parafujo za mwili.(alama 2)

10. Tumia neno “mpaka” katika sentensi kueleza dhana ya: (i) Wakati (alama 1) (ii) Mahali (alama 1) (iii) Kiwango (alama1)

11. Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha pekee ‘o-ote’ katika ngeli ya u-u. (alama 1)

12. **Neno ‘huyu’ limetumikaje (kumaanisha nini katika sentensi hizi)** (alama 2)
(i) Huyu amekuja kwangu. (ii) Mgeni huyu amekuja kwangu

13. **Tunga sentensi ukitumia kielezi cha:** (i) namna/jinsi.(alama 1) (ii) Idadi. (alama 1)

14. **Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.**
i) Alilala jioni. (alama 1) ii) Mchezaji huyu ni hodari sana. (alama 1)

15. **Ziandike** sentensi zifuatazo ukitumia kiwakilishi cha pekee o-ote. (alama 2)
(i) Ufunguo wowote ufunguao ni wetu. (ii) Ngozi zozote zirarukazo ni za kifaru.

16. **Andika** sentensi moja kwa kutumia ‘licha ya’. (alama 2)

17. **Tumia amba katika sentensi hii:** Ua limealo huwa limetiwa mbolea. (alama 1)

18. **Pigia mstari vielezi katika sentensi hizi kisha utambue ni vya aina gani.** (alama 4)
(i) Wezi walipigwa barabara (ii) Wezi walipigwa kwa bunduki

19. **Tunga sentensi moja ukitumia kihusishi cha ‘a’ unganifu** (alama 1)

20. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.
Nomino ya jamii, kirai kihusishi, kitenzi kishirikishi, kielezi cha mahali. (alama 2)

21. Unganisha kwa kutumia kiunganishi cha kinyume. (alama 1) (i) Nitakununulia baiskeli (ii) Sitakupeleka ziara.

22. Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi mwafaka
Utakula limau? Utakula tikitimaji? (alama 2)

23. Tunga sentensi ifuatayo upya kwa kutumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.
Mchezaji alivishwa mtungo mrefu wa maua shingoni baada ya ushindi wake. (alama 1)

24. Tunga sentensi ukitumia ‘A’unganifu mwafaka pamoja na nomino ulizopewa (alama 2)
(i) Teo (ii) Liwali

25. Vitumie vihisishi vifuatavyo katika sentensi. (alama 2)
(i) Ebo! (ii) Kefule!

26. Tumia vivumishi vya pekee kutunga sentensi zenye maana ifuatayo. (alama 2)
(i) bila kubagua (ii)bila kubakisha

27. **Tofautisha sentensi zifuatazo kimaana kwa kuongozwa na vivumishi vilivyopigiwa**

mistari: (i) Mtoto mwenyewe ndiye huyu (ii) Mwenye mtoto ndiye huyu. (alama 2) **28. Tunga sentensi kwa kutumia viunganishi vifuatavyo:-** (alama 4) i) Jinsi ii) Sembuse

29. Kwa kuzingatia upatanishi wa Kisarufi ufaao, tunga sentensi sahihi ukitumia nomino zifuatazo: i) Ulezi ii) Mate (alama 4)

30. Andika sentensi hizi tena bila kutumia kirejeshi "amba"

i) Mtahiniwa ambaye husoma kwa bidii ndiye ambaye hufaulu mtihani wake vizuri. (alama 2) ii) Mtahiniwa ambaye amefaulu vizuri mtihani wake hujiunga na chuo kikuu. (alama 2) **31. Tambua aina za vielezi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo.**

i) Nilipomdai pesa zangu alinijibu kimzahazaha (alama 1) ii) Wanafunzi wanacheza uwanjani (alama 1) **32. Tambulisha** aina za vielezi vya namna katika sentensi zifuatazo. (alama 2) _____(i) Nyanya hutembea kwa mkongojo. (ii) Mwalimu alimkemea kijeshi_____**33**. Tumia 'A' unganifu katika sentensi kudhihirisha matumizi ya: (alama 2)

(i) Kivumishi. (ii) Kiwakilishi

34. Ni hisia zipi zinazodhihirika katika matumizi haya ya vihusishi?

(i) Maskini! Alianguka mtihani wa kitaifa. (ii) Mashala! Mtoto huyu ameuubwa akaumbika.

35. Onyesha kitenzi kikuu na kisaidizi katika sentensi hii. (alama 2)

Nimewahi kumkumbusha makosa yake.

36. Umepewa aina tofauti za nomino. Tunga sentensi idhihirishayo kila aina ya nomino; (alama 3) _____(i) Nomino ya wingi. (ii) Nomino ya kitenzi jina. (iii) Nomino ya kipekee

37. Tumia "O" rejeshi katika sentensi zifuatazo (alama 2)

(i) Mikeka ambayo hufumwa Turkana ni madhubuti. (ii) Uchunguzi ambao wangojewa umewadia._____**38**. Tambulisha viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsi viambata katika sentensi hizi. (alama 3)

(i) Mimi nitakuwa seremala (ii) Akiwa rubani , ataruka kwa ndege

39. Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya-enye na-enyewe (alama 2)_____**40**. Tumia kivumishi kwenye vifungo kukamilisha sentensi:

(i) Tuleteeni ng'ombe yeyote _____ (-dogo) (alama 1)

(ii) Ngoma _____, ndiyo iliyotakikana. (-le) (alama 1)

41.Tumia amba katika sentensi hii: Mtoto anayelia amepigwa na mwizi vibaya sana. (alama 1)_____**42**. Andika sentensi ifuatayo bila kutumia "amba":

Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali. (alama 1)

43. Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea:

Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea. (alama 2)_____**44**. Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi (alama 4)_____(i) Bibi yule alinunua gari _____ (-pya)_____(ii) Mwizi alifukuzwa na mbwa _____ (-angu)

(iii) Mti (-ingine) _____ uliangushwa badala ya ule wa kwanza.

(iv) Nyoka aliingia _____ (-le) shimoni.

45. Tumia kiulizi - pi katika kujaza sehemu zilizoachwa wazi. (alama 4) (i) Ni tunda _____ ulililoleta ?

(ii) Ni mayai _____ yaliyovunjwa ?

(iii) Ni kiwete _____ aliyepata msaada ?

(iv) Ni mitume _____ waliojilolea kufanya kazi ?

46. Andika sentensi zifuatazo bila kutumia neno 'amba'

(i) Jembe ambalo lilinunuliwa jana limevunjika mpini (alama 2) (ii) Mwizi ambaye amekuwa akitusumbua

ameshikwa (alama 2)

47. Unganisha sentensi hizi ili ziweze kuwa sentensi moja.

1. Kelvin ni mwadilifu 2. Kelvin aliteuliwa kuwa kiongozi. (alama 2)

48. Ainisha sentensi hizi (alama 4)

(i) Maji ukiyavulia nguo yaoge . (ii) Twende kwetu sasa hivi

49. Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi ; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.

(alama 4) (i) Anafanya kazi kwa mwajiri wake . (ii) Alifanya mambo kisirisiri.

50. Andika upya sentensi hizi bila kutumia neno amba (alama 4)

(i) Ugonjwa ambao ni hatari sana ni ukimwi .

(ii) Nilimwona simba akinyemelea banda la ng'ombe nilipokuwa nikishika zamu

51.Tumia neno 'mpaka' kama kihusishi cha: (alama 3) (i) Kiwango

(ii) wakati

(iii) Mahali

52. Kamilisha sentensi kwa kutumia vivumishi kama ulivyoagizwa. (alama 3) (i) Rehema ni bibi …… bezo . (umilikaji)

(ii) Naomba kinywaji …… (ziada)

(iii) Muonye bawabu …….. kwa kutofika mapema.(kusisitiza-mbali kidogo) **53**. Ainisha matumizi ya –ema katika sentensi ifuatayo (alama 3) Mwanafunzi mwema ametunzwa vyema kwa wema wake.

54. Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi na kiambishi ngeli.(alama 2) Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

55. Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo. (alama 4) (i) Uhusiano wa zaidi ya hayo

(ii) Kuonyesha chanzo

56. Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi iuatayo

Mama amewahikupika jikoni.

57. Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano.

58. Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:-

Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi

59. Unganisha sentensi hii kwa kutumia *'O'* rejeshi :-

Wavu umekatika. Wavu ni wao.

60. Onyesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani:-

(i) Unamjua vyema kweli? (ii) Hicho wanachokitaka hakipo

61. **Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi**:- (i) Minghairi ya (ii) Wala

62. Eleza maana ya 'jinsi' kama inavyojitokeza katika sentensi zifuatazo

(i) Naomba unionyeshe jinsi ya kuendesha gari

(ii) Wakenya hawapendezwi na jinsi viongozi wanavyoendeleza ufisadi.

63. Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo:-

(i) Wanafunzi wote wameingia darasani. (ii) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani.

64. Tunga sentensi ambayo ina aina za maneno uliyopewa:- N + V + V + T

65. Tumia "O"rejeshi ya kati : Lisemwalo silo liwalo.

66. Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi:-

(i) Bibi yule alinunua gari _____(-pya)

(ii) Mti (-ingine) _____uliangushwa badala ya ule wa kwanza.

67. Pigia mistari chini ya viwakilishi katika sentensi zifuatazo

(i) Ambaye ni mjinga hatafaa kwa shughuli hizi (ii) Nani anaye huzunisha?

68. Bainisha viwakilishi katika sentenzi kisha useme ni vya aina gani?

(i) Mimi nitaondoka kesho. (ii) Huyo alichaguliwa na wengi.

69. Tumia kiulizi kifaacho kukamilisha maswali yafuatayo:

(i) Waashi wale wanaishi kwa (ii) Mtoto alitaka majina… (iii) Wanitania hivyo
70. Tambulisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani?
1.Nani alikukasirisha?... 2. Huyu huwashinda wote
71. Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano
72. Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo: (i) Kishirikishi kipungufu. (ii) Kikuu
73. **Tumia "O" rejeshi katika sentensi hii:** Mwanafunzi ambaye hudurusu ndiye hupita mtihani.
74. **Tumia viunganishi mwafaka kuunganisha sentensi hizi ziwe sentensi moja.**
Alikimbia kwa nguvu zake zote. Alishindwa, kulikuwa na mtu mwenye mbio kumliko.
75. Tumia mzizi -w- katika sentensi kama: (alama 2) (i) Kitenzi kisaidizi (ii) Kitenzi kishirikishi.
76.Tumia kivumishi kionyeshi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya I-ZI kisha utunge sentensi katika ukubwa- wingi
(alama 2) 77. Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya neno: **ilmradi.** (alama 2)
78. Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha bezo
(alama 1) 79. Eleza maana ya sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Tunda lenyewe limeoza. (ii) Tunda lenye shimo halinunuliki.
80. Tunga sentensi ukitumia vihisishi hivi. (alama 2)
(i) Ahaa! (ii) Taib!
81. Tumia –enye au –enyewe kukamilisha sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Shule …… shida daima husaidiwa.
(ii) Kucheza …….. kulikuwa kwa kupendeza.
82. Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo.
Walimu ni watu wasiopendwa wanaposema ukweli kuhusu wanafunzi (alama 3)
83. Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (alama 2)
(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa
(ii) Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.
84. Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (alama 2) Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.
85. Eleza maana ya kihusishi (alama 2)
86. Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo: Mama atasafiri kutoka Ujerumani hadi Ufaransa.(alama 3) 87. Eleza matumizi ya neno mzee katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Baba mzee amelewa (ii) Mzee amelewa
88. Tumia neno 'kuwa' kama kitenzi kishirikishi kikamilifu katika sentensi (alama 1)
89. Tumia amba katika sentensi ifuatayo: Alaye ndiye aliaye (alama 2) 90. Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani.
(ii) Wachezaji wote wameingia uwanjani.
91. Tumia neno 'hadi' kama kihusishi cha; (alama 2)
(i) Wakati (ii) Mahali.
92. Tumia kielezi cha namna kiigizi katika sentensi (alama 2)
93. Tofautisha kati ya vivumishi hivi kwa kueleza maana ya kila kimojawapo (alama 2) (i) -ingine (ii) -ingineo
94. Tunga sentensi mwafaka ukitumia kielezi cha:- (alama 2)
(i) Namna kiigizi (ii) Cha mahali

95. Tunga sentensi yenye fungu tenzi lenye muundo ufuatao : Ts + T + N (alama 2)
96. Unda sentesi yenye muundo ufuatao : KN(N+V),KT(t+ V+E) (alama 2)
97. Ainisha vihusishi katika sentensihii : (alama 3)
Tulichakura tarakilishi ya mwalimu iliyokuwa kando ya dawati baada ya mtihani kukamilika.
98. Tumia kiunganishi seuze / sembuse katika sentensi. (alama 2) 99. Ainisha vitenzi katika sentensi hii.
Hawa ndio wageni tuliokuwa tukingojea kwa hamu. (alama 2)
100. Tumia kihusishi cha wakati kisahihi katika sentensi. (alama 1)
101. Taja uamilifu wa maneno yaliyopigiwa mistari. (alama 3) i. Majisifu ameenda wangwani ii. Hapa ni pangu iii. Haraka yako itakuponza 102. Tumia kiunganishi cha uteuzi katika sentensi. (alama 2)
103. Tumia kivumishi-ingineo katika ngeli ya I-I katika sentensi. (alama 2)
104. Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia kitenzi ndi
Sisi tulipanga mkutano huo. (alama 2)
105. Tumia kirejeshi cha kati kuunganisha sentensi hizi
(i) Mgeni amefika mapema (alama 2) (ii) Mgeni amekaribishwa
106. Tumia kiwakilishi kisisitizi cha nomino uteo katika umoja, katika sentensi. (alama 2) 107. Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kihusishi cha sababu. (alama 2)
108. Andika sentensi yenye muundo ufuatao: KN (W+S) + KT(T+RN (N+V)) (alama 4)
109. Bainisha na uonyeshe aina za viwakilishi katika sentensi zifuatazo
(i) Yule ataajiriwa kazi huko mjini (ii) Cha kuvunda hakina ubani (iii) Wanene watahojiwa
110. Andika sentensi zifuatazo upya ukitumia kirejeshi ‘amba’ (alama 2) (i) Nyoka aliyemuuma punda wangu ameuawa na wanakijiji waliofika kwa wingi. (ii) Mahali palipotayarishwa pamejaa waumini walitoka nchini kote. 111. Ainisha nomino katika sentensi hii; Jopo lilitarajiwa kusema ukweli. (alama 2)
112. Eleza aina ya kielezi kilichopigwa mstari: Kadzo alipambana kiume. (alama 1)
113. Sahihisha bila kuondoa ‘enye.’: Gari lenye lilitujia halikuwa na utingo.
114. Tunga sentensi kwa kutumia nomino ifuatayo katika hali ya wingi. (alama 2)
Uyoga
115. Ainisha vitenzi katika sentensi hii: Ukweli ulio na uchungu haupendwi. (alama 2) 116. Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi: mingairi ya (alama 1)
117. Bainisha vitenzi katika sentensi :
Mtoto wake amekuwa mtukutu ingawa hiyo ni tabia ya babake. (alama 2) 118. Iandike sentensi hii upya kwa kutumia O-rejeshi tamati. Maua ambayo yanapaliliwa hurembesha bustani hii. (alama 1)
119. Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha kulinganisha. (alama 1)
120. Tumia 'o' rejeshi tamati. (alama 2)
Wanafunzi ambao walipita mtihani ni wale ambao walisoma kwa bidii.
121. Tunga sentensi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati.
122. Tunga sentensi yenye kihuhishi cha 'a' - unganifu katika ngeli ya U - ZI. (alama 1) 123. Ainisha chagizo katika sentensi ifuatayo;
Wanafunzi wote waliondoka kwenda nyumbani jana alasiri. (alama 2) 124. Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha masharti, hali timilifu; wakati ujao

(alama 2) (i) Asha na John wamejisajili. (ii) Asha na John watachaguliwa tena.

125. Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi kisisitizi vya ngeli ya KU (alama 2)

126. Tunga sentensi ukitumia nomino yoyote, ukibainisha kiwakilishi cha ngeli. (alama 2)

127. Onyesha kielezi, kivumishi, kitenzi na nomino katika sentensi hii. (alama 4)

Watoto watatu walipeperushwa juu kwa juu na upepo mkali

128. Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Vifaru wote watalindwa kesho.

129. Bainisha aina ya maneno yaliyopigwa mistari katika sentensi zifuatazo.

(i) Nipatie kazi <u>yoyote</u>.

(ii) <u>Yoyote</u> inazidi kulenga juu. (alama 2)